

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Shule ya Sekondari Ipande,

S.L.P 403,

Kyela.

Simu 076677733/0713672257

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.

.....

.....

.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IPANDE WILAYA YA KYELA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka **2021** katika shule ya sekondari Ipande iliyopo katika kijiji cha Mbula kata ya Ipande taarafa ya Ntebela wilaya ya kyela mkoani Mbeya

- i) Shule itafunguliwa rasmi tarehe **11/01/2021** hivyo unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **04/01/2021**.
- ii) Mzazi au mlezi unaombwa kumtayarishia mtoto wako mahitaji yote ili kuondoa usumbufu kwa mtoto wako.
- iii) Mzazi /Mlezi kumbuka kuwa mtoto aliyefaulu kuletwa shuleni ni **lazima** vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa.

SARE YA SHULE

WAVULANA

- a) Suruali mbili (2) Moja rangi ya dark blue na nyingine rangi ya damu ya mzee zisishonwe kwa mfumo wa jinsi na zisiwe za kubana na shati nyeupe mbili za mikono mifupi.
- b) Nguo za michezo yaani Bukta/Traksuti na viatu vya kuchezea.
- c) Viatu vya ngozi jozi mbili nyeusi.

WASICHANA

- a) Suruali mbili, moja rangi ya dark blue nyingine ya rangi ya damu ya mzee zisishonwe kwa mfumo wa jinsi na zisiwe za kubana na blauzi mbili zenye visolo rangi nyeupe.
- b) Rangi ya hijab ni nyeupe.
- c) Jozi mbili za viatu vya ngozi rangi nyeusi na soksi nyeupe na nyeusi.
- d) Visolo viwili kwa wasichana.
- e) Nguo za michezo traksuti na viatu pamoja na T-shirt ya michezo.

MAHITAJI MENGINE YA DARASANI

- a) Daftari kumi (10) yaani counter book (kuanzia 2 quire/3quire na kuendelea) Mkebe(mathematical set), Kalamu za wino na risasi, Rula na dictionary(English-swahili dictionary)